BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 17 Mei, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

80. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Kwa kuwa vijana wenye ulemavu wana haki sawa na vijana wasio na ulemavu.

    Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha vijana wenye ulemavu wanajengewa uwezo juu ya masuali mbali mbali ya kijamii ili waweze kunufaika na fursa za vijana zilizopo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

114. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Eneo la Mwanakwerekwe kuelekea Nyumba Mbili hadi Makaburini, ni eneo lililozungukwa na wajasiriamali wanaofanya shughuli zao za ujasiriamali.

Ni lini Wizara yako itafikiria suala la kuwapatia mikopo nafuu itakayowawezesha kuendelea na shughuli zao za kujiajiri.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

25. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kupitia Sheria Namba 2 ya mwaka 2005 imetoa mamlaka kwa ZSSF kuwekeza fedha zinazokusanywa kwa wachangiaji katika miradi kwa lengo la kufikia nafasi ya ufadhili ya asilimia 100 huku ikipunguza kiwango tete cha michango.

(a) Je, tangu kuanzishwa kwa Mfuko, ni kiasi gani cha fedha kimewekezwa katika miradi ya maendeleo.

(b) Je, katika uwekezaji huo, ni faida gani imepatikana kwa ZSSF na wachangiaji wakuu wa Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii.

(c) Je, ni zipi hasara za uwekezaji huo katika miradi iliyofanywa na ZSSF tokea kuanzishwa kwake.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

120. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni lini hasa Karakana ya Mafunzo ya Amali iliyopo ndani ya skuli ya Mwanakwerekwe ‘A’ itaboreshwa kulingana na mahitaji yake muhimu kwa sasa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

19. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa na Serikali ya kusambaza maji vijijini na ujenzi wa matangi kadhaa, yapo maeneo ambayo bado yana changamoto ya maji kupitia visima na matangi ya maji ikiwemo kijiji cha Sizini, Wilaya ya Micheweni.

    (a) Ni lini Serikali itawachimbia kisima chengine cha kisasa wana Sizini ili waweze kuondokana na changamoto inayowakabili kwa sasa.

    (b) Ni lini Serikali itawajengea tangi la maji ili nao waweze kupata maji safi na salama kwa uhakika.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

274. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

     Ni ipi kauli mbiu ya Shirika la Utangazaji Zanzibar na tathmini ya utekelezaji wake ikoje kwa sasa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

246. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

     Nawapongeza viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa jinsi wanavyotujengea barabara za ndani katika jimbo la Nungwi. Kiujumla barabara zote zimejengwa kwa kiwango cha lami lakini kuna changamoto ya watu kupata ajali za mara kwa mara hasa katika barabara za ndani.

     Kutokana na ajali kuongezeka kila uchao, Je, ni lini Wizara yako itaweka matuta katika barabara hizo ili kupunguza ajali.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2025/2026.

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
17 Mei, 2025.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA**